

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA SABA

28 APRILI, 2016



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA SABA – TAREHE 28 APRILI, 2016

I. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

II. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

61. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX
(VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-
Kumekuwa na ongezeko la ombaomba au
utegemezi kwa wenye ulemavu nchini:-

Je, ni kwa nini Serikali isiwawezeshe kiuchumi
watu wenye ulemavu kwa kuwapa upendeleo wa
zabuni za kazi mbalimbali kama vile kuzoa taka,
usafi wa vyoo, ushonaji n.k kwenye kila
Halmashauri.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

62. MHESHIMIWA KEMIREMBE JULIUS LWOTA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI:-

Je, ni lini Serikali itapeleka X – Ray na CT – SCAN kwenye hospitali ya Sekou Toure Mkoani Mwanza.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

63. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Ingawa kuna tatizo la ajira Serikalini, lakini inasemekana kuwa ziko nafasi nyingi zilizo wazi katika ngazi ya Wizara, Mikoa, Wilaya hata Vijiji:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali inalificha jambo hili na ni lini sasa itajaza nafasi za ajira zilizo wazi katika maeneo mbalimbali ikiwemo Halmashauri ya mji wa Mbulu katika Sekta za Utawala kama vile VEO, WEO ambapo wananchi huwalipa watumishi wa kukaimu kwa fedha zao wenyewe kinyume na taratibu;

(b) Je, ni kwa nini Serikali isipandishe mishahara ya kima cha chini kwa kuzingatia mahitaji ya maisha ya sasa.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

64. MHESHIMIWA SUSAN ANSELM LYIMO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:- Mwaka 2015 Haki Elimu walitoa tathmini ya utafiti wa elimu kwa kipindi cha miaka 10 ya Awamu ya Nne na kugundua ongezeko kubwa la udahili kwa ngazi zote na kuporomoka kwa ubora wa elimu:-

- (a) Je, ni kwa kiasi gani utafiti huo umeakisi uhalisia wa hali ya elimu hususan ile ya Sekondari;
- (b) Je, Serikali ya Awamu ya Tano ina mikakati gani ya kuinua ubora wa elimu hapa nchini.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

65. MHESHIMIWA JUMA KOMBO HAMAD (WINGWI):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Serikali imekuwa ikiendeleza zoezi la bomoa bomoa katika maeneo tofauti hapa nchini; zoezi hili limekuwa likiwaathiri Wananchi kiuchumi na hasa kisaikolojia kwa kuwaacha wakiwa hawajui waelekee wapi:-

Je, kwa nini Serikali isiwapidie Wananchi hawa hasa ikizingatiwa kwamba wakati wanajenga Serikali ilikuwa inawaona lakini haikuchukua hatua stahiki.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS: (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA)

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.



(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
28 APRILI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**